JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Tanzania Kuendeleza Ushirikiano wa Kidiplomasia na Jumuiya ya Kimataifa

**Dar es Salaam, 28 Novemba 2025**
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mahmoud Thabit Kombo (Mb.), leo Ijumaa tarehe 28 Novemba, 2025 amekutana na Jumuiya ya Wanadiplomasia (Diplomatic Corps) wanaowakilisha Mataifa na Taasisi za Kimataifa nchini. Mkutano huu ni wa kwanza tangu kuundwa kwa Serikali mpya ya awamu ya sita kipindi cha pili kufuatia uchaguzi mkuu wa Oktoba 2025.

Katika kikao hicho, Waziri Kombo amewahakikishia Mabalozi ushirikiano wa Tanzania kwa nchi zao na mashirika wanayowakilisha. Kwa upande wao, Mabalozi hao wamethibitisha dhamira yao ya kuendelea kushirikiana na Tanzania, ambapo Waziri amesema ni kielelezo cha ukomavu wa diplomasia, pamoja na uhusiano imara baina ya Tanzania na washirika wa maendeleo.

Aidha, kupitia mkutano huo, Serikali ilitoa taarifa kwa Mabalozi kuhusu zoezi la uchaguzi kwa ujumla na matukio mengine yaliyojiri tarehe 29 Oktoba, 2025. Pamoja na vurugu zilizojitokeza, Serikai imewafahamisha wanadiplomasia hao hatua zilizofuata, ikiwemo kurejesha hali ya utulivu na maisha ya kawaida, ulinzi wa maisha na mali za wananchi, pamoja na kuhakikisha mwendelezo wa huduma za miundombinu ya umma na shughuli za kiuchumi. Waziri pia ameeleza kuhusu Tume ya Uchunguzi iliyoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini chanzo cha matukio hayo na kuja mapendekezo ya hatua stahiki za kuimarisha mifumo ili kuzuia matukio kama hayo yasijirudie.

Aidha Waziri amewafahamisha Mabalozi kuwa Tanzania imepitia katika kipindi kigumu ambacho hakijawahi kutokea katika historia yake. Pamoja na changamoto hii, Serikali na Watanzania kwa ujumla sasa wanaingia kwenye hatua ya kuliponya taifa na kudumisha umoja, undugu na mshikamano ili kusonga mbele. Serikali itahakikisha tathmini ya kina na hatua muhimu zinachukuliwa, zikiwemo majadiliano, uwajibikaji na uimarishaji wa taasisi, ili kuhakikisha matukio ya namna hiyo hayajirudii tena.

Tanzania inaelewa kuwa wadau mbalimbali wamekuwa wakitoa matamko kuhusu hali ya Tanzania na inawaasa na kuwasihi kuipa Tanzania nafasi ya kukamilisha uchunguzi iliouanzisha. Wngi wa matamko haya yanaweza kuwa sehemu ya kupotosha au kuharibu uchunguzi husika. Tunaheshimu uhuru, lakini tunazingatie uhuru wenye mipaka na uwajibikaji. Kama ilivyo historia yake, Tanzania ni muumini wa ushirikiano wa pamoja kimataifa wenye kuleta tija kwa pande zote, amani na maendeleo.

Kuhusu Bunge la Umoja wa Ulaya, Waziri amebainisha kuwa Tanzania imefuatilia maazimio ya Bunge hilo, na kwamba imemuelekeza Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mjini Brussels kuendelea na mashauriano ya kidiplomasia na taasisi za Umoja wa Ulaya na wadau husika, ili kuimarisha ushirikiano na kuendeleza maslahi ya pamoja ya amani, utulivu na ushirikiano.

Imetolewa na;
Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali